TANGAZO LA SERIKALI NA. …….la tarehe ……..

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

Zimetungwa chini ya vifungu 6(1) na 16 (1)

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA ZA MWAKA, 2014

Jina na mwanzo wa kaunza kutumika

1 Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka 2014 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2 Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Manispaa ya Tabora

Tafsiri

3 Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"*Afisa Muidhiniwa***"** maana yake ni Afisa yeyote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"*Halmashauri***"** maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Tabora.

*"Hesabu***"** ina maana ya jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada, katika mwaka wa mapato;

"*Hesabu za mwisho"* ina maana ya hesabu za mwisho zinazowasilishwa na Taasisi yoyote ya kibiashara au mfanyabiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa aya ya 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"*Jumuisho***"** ina maana ya taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yoyote yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho;

"*Kipindi cha hesabu***"** ina maana ya muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

"*Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"*Mkusanya kodi***"** maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa na Halmashauri kukusanya kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"*Mwaka wa mapato***"** maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"*Sheria"* maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290.

*"Taasisi ya kibiashara***"** ina maana ya taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au Sheria ya Majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Utozaji wa kodi

4 (1) Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara na kwa kila mfanyabiashara katika kila Mwaka wa Fedha ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

(2) Matawi ya makampuni yanayofanya biashara katika eneo la mamlaka ya Halamshauri yatatakiwa kulipa ushuru wa Huduma katika Halmashauri husika.

Uwasilishaji wa taarifa kuhusu shuhguli za biashara

5 Mkurugenzi kwa taarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha hesabu zenye taarifa kamili za shughuli za kibiashara zikionesha kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kuingizwa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

Uwezo wa Mkurugenzi kumtaka mtu yeyote

6 Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu yeyote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yoyote ya kibiashara inayopaswa kulipa kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi

kuwasilisha taarifa

kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.

Uwezo wa kuingia kwenye jengo

7 Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Muidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la Taasisi ya kibiashara au la mlipa au mkusanya kodi yeyote kwa nia ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanya kodi hiyo.

Kuwasilisha kumbukmbu za biashara

8 -(1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipa kodi au mkusanya kodi yeyote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya kodi ya huduma.

-(2) Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya (1) Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu yeyote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

Muda wa kulipa

9 Mlipa ushuru wa Huduma au mkusanya ushuru huo atatakiwa kuwasilisha taarifa juu ya kiwango cha mapato yake na kulipa ushuru kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa hapa chini;-

(a) Kwa wale wote ambao wanafanya biashara ya kuingiza bidhaa toka nje ya nchi, watalipa kulingana na wanavyolipia ushuru wa Forodha kama ilivyoainishwa na Kamishna wa Forodha.

(b) Kwa wale wote ambao wamejiandikisha kulipa Kodi ya ongezeko la Thamani (VAT) watalipa kama wanavyolipia kodi hiyo ya ongezeko la thamani (VAT).

(c) Walipa ushuru wengineo, watalipa kodi hii kwa awamu nne sawa, awamu ya kwanza ikiwa ndani ya miezi mitatu kuanzia mwanzo wa mwaka unaohusika.

Uteuzi wa mkusanya kodi

10 (1) Halmashauri inaweza kukasimu madaraka kuwateua Kamishna wa Kodi ya Mauzo ya ongezeko la Thamani (VAT), Kamishna Kodi ya Forodha au Kamishna wa Kodi ya Mapato kuweza kukadiria na kukusanya ushuru huu wa huduma kutoka kwa mlipa ushuru wa huduma au wakala wake kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo ya 9 ya

Sheria Ndogo hizi, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa Kamishna wa Ushuru wa Forodha atatozwa asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya bei ya kiwandani pamoja na Kodi zote isipokuwa VAT.

(b) Kwa Kamishna wa kodi ya uongezeko la Thamani (VA) atatoza asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya bei ya Kiwandani pamoja na Kodi zote isipokuwa VAT.

(c) Ikiwa ni Kamishna wa Kodi ya Mapato atatoza asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya mapato yote ghafi.

(2) Bila ya kuathiri maelezo ya Sheria Ndogo ya 10 (1) ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza akamteua Kamishna wa Kodi ya Mapato kukadiria na kukusanya Kodi zote ambazo muda wake wa kulipa utakuwa tayari.

(3) Mlipa ushuru yoyote atakayeshindwa kuwasilisha ushuru atakuwa ametenda kosa na atawajibika kulipa ushuru huo kama deni kwa Halmashauri na hatua zote za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kama mlipa kodi.

(4) Bila ya kuathiri Sheria Ndogo ya 10 (1) ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kumteua au kuwateua mtu, au kikundi cha biashara kuwa wakala wa ukusanyaji wa ushuru huo na litakuwa ni jukumu la mtu huyo kufanya mambo yafuatayo:-

(a) Kuwasilisha habari na kumbukumbu zote za shughuli za biashara kama ilivyoainishwa na Sheria Ndogo hizi;

(b) Kuandaa na kuwasilisha makadirio ya ushuru na kulipa ushuru huo kwa Halmashauri kama ilivyoainishwa na Sheria Ndogo ya 9 (C) na 12 (1).

Kiwango cha ushuru

11 (1) Kiwango cha kodi kitakuwa ni Asilimia sifuri nukta tatu (0.3%) ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

(2) Mkusanya kodi au mlipa kodi yeyote akishindwa kuwasilisha kodi yake au ya mlipa kodi, atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kuwajibika kulipa kodi hiyo kama vile ndiye mlipa kodi ya Halmashauri, na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kuteua Wakala kukusanya kodi kwa niaba yake na Wakala huyo atakuwa na jukumu la:-

(a) kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa Muidhiniwa; na

(b) kuwasilisha kodi aliyokusanya katika kipindi maalum

Wajibu wa mlipa ushuru na mkusanya ushuru

12 (1) Kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi mine tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.

(2) Mlipa kodi au mkusanya kodi anapowasilisha hesabu zake, Afisa Muidhiniwa anaweza:-

(a) kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathmini kodi katika msingi huo; na

(b) kufanya tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa kodi huyo iwapo ataamini kuwa kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

(3) Kodi iliyotathminiwa kwa mujibu wa Sheria ndogo hizi, italipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

Utozaji wa riba

13 (1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia kumi na tano (15%) kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi inayodaiwa.

(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama kodi inayolipwa na mlipa kodi huyo.

Tozo na adhabu

14 Mtu yeyote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa mwezi au shilingi Elfu Hamsini (50,000/-) kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.

Makosa na adhabu

15 Mtu yeyote ambaye;-

(a) Atashindwa kuwasilisha Taarifa ya Mapato yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(b) Atashindwa kuwasilisha habari, kumbukumbu, nyaraka ambazo alitakiwa kuwasilisha Halmashauri;

(c) Atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;

(d) Atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa Halmashauri katika muda uliowekwa;

(e) atashindwa kutunza hesabu ya shughuli zake kwa mujibu wa Sheria au kanuni za kihasibu;

(f) Atamshawishi mtu yeyote asilipe au atamzuia mkusanyaji ushuru wa huduma kufanya kazi yake;

(g) atashindwa kutoa nyaraka au taarifa yoyote ile itakayotakiwa na Halmashauri wakati wa ukaguzi;

(h)

(i) Atakuwa ametenda kitendo chochote ambacho ni kinyume cha Sheria Ndogo hizi,

(j)

Atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi Shilingi Elfu Hamsini (50,000/= au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo

Kufifilisha kosa

16 Mkurugenzi atakuwa na Mamlaka ya kufifilisha kosa ikiwa mkosaji atakiri kwa maandishi kufanya kosa, baada ya kukiri kufanya kosa atatozwa faini isiyozidi Elfu Hamsini, Ushuru wote anaodaiwa, pamoja na tozo la asilimia 30%.

JEDWALI

FOMU YA KUFIFILISHA KOSA
(Chini ya kifungu cha 16 cha Sheria Ndogo hizi)

Mimi …….. wa S.L.P. ……. Ninaefanya biashara ya …… katika eneo la …….. lililopo ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Tabora. Nakiri kuwa leo tarehe ……. nilikiuka kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Manispaa ya Tabora za mwaka 2014. Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwiapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 18 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini ……..

Mbele yangu ……. (jina)

Saini ……..

Wadhifa ……